
# YESU KATIKA INJILI YA YOHANA



# YESU KATIKA INJILI YA YOHANA

Kimeandikwa na Ann Berkley, Josphat M.M.Gikiri,
Bernard Kabaru Mwangi and Paul G. Karani

**BIBLE STUDIES FOR AFRICAN YOUTH**

Africa Coordinated Curriculum
for Bible Study

Y1 - 2Ps
Used with permission of
International Publications Services

Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI

© Copyright , 1988
Baptist Publications House
All Rights Reserved

6. Omba kwamba utashiriki kwa haki ujumbe huu na rafiki zako na uwe tayari kuhubiri Injili ya Kristo aliyefufuka kwa watu wote.

ndivyo Wakristo wote wataishi pamoja na Yesu kule mbinguni jinsi ilivyoandikwa katika 1 Wathesalonike 4:16-17.

Mariamu Magdalena aliende kaburini wakati wa mapambazuko. Kwa Wakristo, mapambazuko ni ishara ya tumaini. Hutupa picha ya wakati ambapo tutafufuka na tupate uzima wa mbinguni jinsi ilivyoandikwa katika Marko 16:2. Tutafufuliwa katika uhai mpya. Watu wote wanapaswa kuweka imani yao katika Yesu na wawe na uhakika wa kuishi naye baada ya kufufuliwa miili yao jinsi mtume Yohana alivyokuwa.

Wakristo wanapaswa kuhubiri Injili ya Yesu Kristo kwa sababu yu hai. Ikiwa Kristo hakuwa amefufuka, basi imani kwake haingekuwa na mwanzo, kusudi au mwisho ambao ingeelekezewa. Yesu yu hai na anaendelea kutuongoza kupitia kwa Roho Mtakatifu ambaye alituahidi. Roho Mtakatifu aliyeahidiwa anaishi ndani yetu nasi twafurahi kwa sababu Yesu anaishi ndani ya mioyo ya watu wake.

**Kazi ya Kufanya**

1. Kwa nini wanafunzi walifikiria kwanza kwamba mwili wa Yesu ulikuwa umeibiwa?

2. Je! ni nini kilichowafanya wanafunzi kuwa na hakika kwamba Yesu hakuwa ameibiwa lakini alikuwa amefufuka katika wafu?

3. Je! ni nini kinachowafanya Wakristo kuwa na tumaini la kuishi tena baada ya kufa?

4. Yesu yu hai hata sasa. Je! watu wanapaswa kuwa na nini ili nao waishi pia?

5. Omba kwamba utakuwa na imani katika Bwana aliye hai na umwamini kwa kukupa uzima baada ya kufa.



## YALIYOMO

**SURA** **UKURASA**


1. Yesu Hapo Mwanza. ........ 5
2. Yesu Anaanza Huduma Yake. ........ 9
3. Yesu Anathibitisha Uwezo Wake. ........ 13
4. Yesu Anafundisha Kuhusu Kuzaliwa Upya. ........ 17
5. Yesu Anawashuhudia Wenye Dhambi ........ 21
6. Mamlaka ya Yesu. ........ 26
7. Maneno ya Uzima wa Milele. ........ 31
8. Yesu Bwana wa Mauti. ........ 35
9. Kristo Mwenye Ushindi ........ 39
10. Yesu Anamtuma Mfariji ........ 43
11. Yesu Anasalitiwa na Kukanwa. ........ 47
12. Yesu Anasulibiwa ........ 51
13. Yesu Yu Hai. ........ 55

## KUHUSU WAANDISHI

Kitabu hiki kimeandikwa na Ann Berkley, Josphat M.M. Gikiri, Bernard Kabaru Mwangi na Paul G. Karani.

Bi. Berkley ni mwalimu mmisheni wa Nyeri Baptist High School, Nyeri, Kenya. Yeye na mumewe, Clyde, wana mabinti wawili. Naye ni mshiriki wa Nyeri Baptist Church.

Bw. Gikiri ni mwalimu pia. Anafanya kazi na vijana wa wilaya ya Murang'a (Kenya) na ni mwenye kiti wa Idara ya vijana Wabatisti. Yeye ni mshiriki wa Kaimiri Baptist Church.

Bw. Mwangi anahudumia vijana wa Kiangondu Baptist Church katika eneo la Nyeri. Amewahi kufanya kazi na vijana wa kanisa lake, jumuiya ndogo na Kenya nzima.

Bw. Karani ni mwalimu wa watu wazima. Amewahi kufanya kazi na vijana kwa muda wa miaka kumi. Yeye ni mshiriki wa Ziyobomu Baptist Church, Malindi, Kenya.

kubashiri kwake kwamba angekufa na kufufuliwa katika wafu jinsi ilivyoandikwa katika Luka 24:7.

Kufufuka kwa Yesu kunaonyesha kwamba alikuwa mshindi juu ya dhambi, Shetani na mauti, na sasa yu hai.

Baada ya kufufuka kwake, aliwatokea wanafunzi wake mara nyingi. Mara tu alipowatokea, walitambua kwamba Bwana wao amefufuka nao wakajazwa na furaha.

Wakati ulifika ambapo alipaswa kupaa na kwenda mbinguni. Alitaka kuhakikisha kwamba kazi yake itaendelea. Kwa hivyo alimwuliza Petro iwapo anampenda. Twaona katika Yohana 21:15-17 kwamba Yesu alimwagiza Petro kuwalisha wana-kondoo wake baada ya kila kukiri kwa upendo ambako Petro alisema.

Kufufuka kwa Yesu kulileta tumaini la uzima baada ya kifo. Yesu alikuwa amepaa mbinguni na anaishi katika mkono wa kuume wa Mungu Baba.

**Mafunzo ya Sura Hii Kwangu**

Yesu Kristo alikufa na akafufuka. Hili ni tendo la faraja kwetu sisi tunaomwamini kwamba nasi pia tutafufuliwa na kuishi milele.

Mwili wa Yesu uliomfu ambao uliwekwa kaburini usiku ulipata uzima na kuwa hai. Katika kufufuka kwake kuna ahadi ya kufufuka kwetu na kuwa hai. "Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa" (1 Wakorintho 15:22).

Kila mara wakati Bwana aliwatokea wanafunzi wake walijawa na furaha. Wakristo watakuwa na furaha na watafufuka pia wawapo na imani katika yeye aliyefufuliwa. Sisi tutaenda mbinguni wakati Kristo arudipo mawinguni na baada ya sisi kufufuka. Jinsi Kristo alivyopaa mbinguni na anaishi na Baba,

ulikuwa umefurika na hata sasa kulikuwa kungali na maji mengi.

Petro alikufa moyo alipofika pale mtoni. Hakuamini kwamba angeweza kuvuka. Alirudi nyumbani kwa mjomba wake na akamwambia kuhusu hatari ya kuuvuka mto ule. Mjomba yake alimhakikishia kwamba wataweza kuuvuka. Petro hakuwa akiamini kamwe, kwa hivyo aliangalia tu kuona kile ambacho mjombaye atafanya. Mjomba huyo alienda hatua chache kutoka pale walipokuwa na akauvuka mto huo. Petro alipomwona kuwa amevuka kwa usalama naye pia alivuka.

**Maelezo**

Yesu Kristo alikuwa amefufuka katika wafu wakati Mariamu Magdalena alipofika kaburini. Ilikuwa asubuhi mapema alipokwenda kaburini, na mwili wa Bwana wake haukuwepo. Alifikiria kwamba pengine mtu ameuiba mwili wa Kristo.

Alienda kwa haraka na kuwaambia Petro na Yohana kwamba Kristo hayumo tena kaburini. Hawakuamini kamwe walipoambiwa hivyo, basi nao pia wakaenda kaburini. Lakini Yohana aliamini alipoangalia ndani ya kaburi na kuona tu nguo tupu na shuka iliyowekewa kichwa cha Yesu. Mwili ambao shuka hizo zilikuwa zimeufunika haukuwepo, nao wakashawishika kwamba hakuna mtu aliyezishika. Waliamini kwamba Kristo alikuwa amefufuka katika wafu. Soma Yohana 20:8.

Hata ingawa wanafunzi waliamini kwamba Yesu alikuwa amefufuka, hawakuweza kuelewa jinsi ilivyofanyika. Mwili wa Yesu ulikuwa umefufuka jinsi ambavyo hapakuwa na ye yote wa kuweza kuelezea. Mariamu alipokuwa akilia kando ya kaburi, Yesu alimtokea, na aliamini kabisa na akawaambia wengine habari za Yesu Kristo. Imani ya wanafunzi ilikuwa kuu wakati Yesu alipofufuka kwa kuwa walikumbuka





# YESU HAPO MWANZO

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitamruhusu Yesu awe nuru ya maisha yangu.

SOMO KUTOKA: Yohana 1:1-18

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 1:1-5, 9-14

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu" (Yohana 1:1).

**KUSOMA SOMO**

**Utangulizi**

Mwandishi atakapo kuandika historia ya mtu, huanza na wakati alipozaliwa. Ikiwa umesoma maisha ya Yesu katika kitabu cha Mathayo na Luka, unajua kwamba vitabu hivi vinaanza na habari ya kuzaliwa kwa Yesu. Baadhi ya waandishi huanza na tukio muhimu katika maisha ya mtu, na hivi ndivyo Marko alivyoanza. Lakini Yohana alienda zaidi ya kuzaliwa kimwili kwa Yesu kule Bethlehemu. Alianza na jambo la kwanza alilolifahamu kuhusu Yesu. Yohana anatwambia kwamba Yesu alikuwa na Mungu baba wakati wa kuumba na kwamba alifanyika mwanadamu na kuishi hapa duniani. Yohana anatwambia pia sababu iliyomfanya Yesu kuja kuishi duniani.

**Maelezo**

Soma Yohana 1:1-5. Mungu alitaka kuwasiliana na kiumbe chake tangu mwanadamu alipoumbwa. Kabla ya mwanadamu

kutenda dhambi, Mungu alinena naye uso kwa uso. (Mwanzo 3:8) Hatimaye Mungu alinena kupitia kwa viongozi wakuu kama Musa na manabii kama Isaya. Lakini hii haikuwa njia nzuri ambayo Mungu angejidhihirisha wazi kwa mwanadamu. Watu hawa walisema tu habari za Mungu. Alikuwa ameahidi tangu mwanzo kwamba angemtuma yule ambaye angewadhihirishia wanadamu utu wa Mungu. Kwa hivyo Yesu akaja. Yohana anamwita "Neno." Yesu, kama neno, ni dhihirisho halisi la Mungu. Hebu tuone thibitisho la Yohana kwamba Yesu ni Mungu.

1. Alisema kwamba Yesu alikuwepo tangu mwanzo. Hakuwa na mwanzo. Yeye ni Mungu.

2. Yesu ndiye aliyeumba vitu vyote. Alikuwa pamoja na Baba wakati vitu vyote vilipoumbwa.

3. Yesu ni nuru na uzima. Uzima ambao Yesu anatoa ni mkuu, wenye maana sana, uzima wa milele. Yesu alikuja kama nuru yetu, nuru inayowaonyesha watu njia ya uzima. Nuru hii ni kuu sana kwamba hakuna kitu kiwezacho kuizima. Yeye ni nuru ya ulimwengu wote, kwa wote ambao watampokea.

Watu walimkubalije Yesu? Soma Yohana 1:9-13. Hata ingawa Yesu ni utu wa Mungu, Nuru ya kweli, Muumba wa ulimwengu, watu wengi hawakumkubali. Hata ni jambo la kushangaza sana kwamba kabila lake mwenyewe, Wayahudi, watu waliochaguliwa na Mungu hawakumkubali. Yohana alionyesha mifano mingi ya kukataa kwa Wayahudi katika kurasa za kitabu chake. Lakini sio wote waliomkataa Yesu.

Kifungu cha 12 kinaweza kuwa ushuhuda wa Yohana mwenyewe jinsi Yesu alivyomwokoa. Kila mtu aliyemkubali Yesu kama Kristo, aliyemwamini kwa kumwokoa, alifanyika mwana wa Mungu. Yohana alionyesha jinsi wokovu uwezavyo



3. Je! maneno haya, "Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu" yanakuonyesha nini kuhusu tabia ya Yesu ya kumwokoa mwanadamu?

4. Omba kwamba Bwana akuongoze uelewe kwa ukamilifu kwamba alikufia.

5. Omba kwamba utapata nafasi ya kuwashuhudia wengine kwa nini Yesu alipaswa kufa.

SOMO LA KUMI NA TATU

# YESU YU HAI

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba Yesu ni Mwokozi wetu kwa sababu yeye yu hai, hata mimi nitakuwa hai pia.

SOMO KUTOKA: Yohana 20-21

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 20:1-10; 21:15-17

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala" (1 Wakorintho 15:20).

**KUSOMA SOMO**

**Utangulizi**

Wakati wa msimu wa mvua Petro alihitaji kuvuka mto ili aweze kupata gari la kumpeleka nyumbani. Alikuwa amemtembelea mjomba wake aliyeishi karibu na mto. Mvua ilikuwa imenyesha nyingi siku kadhaa zilizopita nao mto

Yesu alijitoa kwa kupenda ili afe badala yetu. "Yesu akalia kwa sauti kuu, akasema, Ee Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu. Alipokwisha kusema hayo alikata roho..." (Luka 23:46-47). Hivi ndivyo alivyofungua njia ya kwenda mbinguni kwa wale wote ambao wamemwamini. Twaona katika Mathayo 27:51, kwamba pazia la hekalu lilipasuka vipande viwili wakati wa kufa kwa Yesu. Hii inamaanisha kwamba njia ya kwenda mbinguni ambayo hapo mbeleni ilikuwa imezuiwa na dhambi zetu sasa ilikuwa wazi. Yesu alirudisha urafiki wetu na Mungu. Yesu alifanya hivi kwa sababu hakuwa na dhambi na alikuwa ndiye wa pekee wa kumwokoa mwanadamu. Soma Matendo 4:12. Hii inatufundisha pia kwamba tunapaswa kujaribu kuishi bila dhambi ili watu wengi wapate kuja kwa Bwana waonapo maisha yetu.

Hapo mbeleni Yusufu wa Arimathea na Nicodemus walionekana wakiwa wafuasi wa siri wa Yesu. Lakini twaona katika Yohana 19:38-42 wakija kwa ujasiri na kutaka mwili wa Kristo. Wakati mwingine Wakristo huogopa Ukristo wao. Tunapaswa kudai bila hofu kwamba Yesu alifia dhambi zetu na tushuhudie ulimwengu kwa ujasiri kuhusu mpango wa Mungu wa wokovu ambao ametupatia.

Yesu alikufa na akaishi tena. Hii inatusaidia kujua kwamba yeye yu Bwana wa watu wote, walio wafu na hai. Kusulibiwa kwake kulileta wokovu kwa wote ambao wangemwamini. Kufufuka kwake ndio msingi wa uzima wa milele.

**Kazi ya Kufanya**

1. Hapo kale watu walitoa dhabihu ya wanyama kama malipo ya dhambi. Je! kwa nini ilimpasa Yesu kufia dhambi za ulimwengu wote?

2. Yesu alipokuwa yungali msalabani alisema kwamba, "Imekwisha." Je! hii inamaanisha nini kwako?



kupatikana tu kwa Mungu alipoandika kwamba, "...aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu...(Yohana1:12)." Yohana alieleza tendo hili kama kuzaliwa. Ni kuzaliwa, "...si kwa damu , wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu" (kifungu cha 13). Ni Mungu tu awezaye kutuzalisha upya. Uzao huu mpya huja tu kwa kuamini na kukubali karama ya Mungu ya wokovu.

Yesu alikujaje duniani? Soma Yohana 1:14. Baadhi ya watu wa wakati wa Yohana wanaamini kwamba Yesu alikuwa Mungu, wala siyo mtu kamili. Hatuwezi kuelewa jinsi alivyokuwa Mungu na mwanadamu lakini ni lazima tukubali ukweli unaomhusu hata ingawa hatuelewi kabisa.

**Mafunzo ya Sura Hii Kwangu**

Yesu alizungumzia juu ya Yesu kama nuru. Je! umewahi kufikiria jinsi nuru ilivyo muhimu? Mimea haiwezi kukua bila nuru. Ikiwa jua halingeangaza, basi hatungekuwa na mimea wala chakula. Tunahitaji nuru kuweza kuona. Iwapo hakungekuwa na nuru, hatungehitaji macho. Hakungekuwa na kitu cho chote cha kuona.

Tunahitaji pia nuru kwa afya ya roho zetu. Roho zetu ni muhimu sana kuliko miili yetu ambayo utakuja kufa. Tunahitaji nuru rohoni mwetu kutuonyesha ukweli wa maisha. Yohana alimwita Yesu, "Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu."

Mfikirie Yesu kama nuru itusaidiaye kuona mambo haya:

1. Yesu hutusaidia kumwona Mungu, na kujua kwamba yupo. Maisha yake hapa duniani yalikuwa njia ya Mungu ya kujidhihirisha kwetu.

2. Nuru ya Yesu hutuonyesha ukweli. Hutusaidia kuuona ulimwengu jinsi ulivyo, wenye dhambi na unao kufa. Hutusaidia kuona suluhisho la Mungu kwa dhambi.

3. Yesu hutusaidia kujiona sisi wenyewe kama watu wenye dhambi wahitajio Mwokozi.

4. Yesu huongoza njia yetu tunapoenenda maishani. Yeye ni kama kurunzi inayotwonyesha mahali pa kukanyaga na pale pa kuepuka. Hatutakuwa na shida nyingi maishani tukiifuata nuru yake.

5. Nuru ya Yesu hutulinda. Huzuia mambo yasiyojulikana gizani. Hutuondolea hofu.

6. Nuru ya Yesu hutusaidia kuwaona wengine na mahitaji yao. Tunaweza kuona njia nyingi za kuwasaidia watu wengine tunapouangalia ulimwengu kupitia kwa nuru ya Yesu Kristo.

Je! umezaliwa katika jamaa ya Mungu? Yohana 1:12 inatwambia kwamba tukimpokea, tukiliamini jina lake, tutafanyika washiriki wa jamaa yake. Tufanyapo hivyo, Yesu atakuwa nuru tunayohitaji maishani.

**Kazi ya Kufanya**

1. Taja thibitisho tatu ambazo Yohana anatoa kwa kusema kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu.

2. Je! ni watu gani ambao hawakumkubali Yesu kama Mwana wa Mungu?

3. Mtu anawezaje kufanyika mtoto wa Mungu?

4. Yohana anaelezeaje kuhusu kuzaliwa kwa Yesu?

5. Orodhesha baadhi ya mambo ambayo nuru hukufanyia. Je! kungefanyika nini maishani mwako ikiwa Yesu ndiyo nuru yako?



akasema, "...Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!" (Yohana 1:29).

Yesu alikufa ili kuwaokoa wenye dhambi. Hakuamua kujiokoa yeye mwenyewe kwa sababu hiyo hangemwokoa mtu ye yote. "Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu" (Yohana 12:32). Alikuwa mwana-kondoo aliyetolewa kama dhabihu. Usemi huu, "Imekwisha," ulitumiwa wakati wa kununua na kuuza bidhaa. Yesu aliposema maneno haya katika Yohana 19:30, alimaanisha kwamba alikuwa amelipa deni lote la ukombozi wa mwanadamu kutoka kwa dhambi zake. Yesu alikuwa amehubiri, amefundisha, ameponya na kuwafufua watu. Sasa damu yake ilikuwa imemaliza kazi ya wokovu. Yesu alipatwa na kiu alipokuwa msalabani. Mtu mmoja alitia sifongo katika siki na kumpa Yesu badala ya kumpa maji kwa ajili ya kiu.

Watu waliomsulubisha Yesu hawakujua kile walichokuwa wakifanya. Yesu alikuja kumwokoa mwanadamu kutoka dhambini, lakini alisulibiwa kama mhalifu. Ilikuwa imeandikwa kwamba atakufa msalabani. Hii ndiyo sababu aliposema, "...Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo" (Luka 23:34).

Baada ya Yesu kusulibiwa na kufa, kulifanywa matayarisho ya mazishi yake, na alipelekwa kaburini. Soma Yohana 19:38-42. Hata hivyo, angefufuka ili ampe mwanadamu tumaini la uzima wa milele.

**Mafunzo ya Sura Hii Kwangu**

Yesu alikuwa kama Stefano katika Utangulizi wa somo hili. Sisi sote tulikuwa kama Marko ambaye hakumtii Baba yake. Yesu alikufa badala yetu. Hatungeweza kulipia dhambi zetu lakini Yesu, kama Stefano alituonea huruma na akachukua adhabu ya dhambi. Tulipaswa tufie dhambi zetu wenyewe.

**KUSOMA SOMO**

**Utangulizi**

Mtu mmoja alikuwa na wana wawili wa kiume. Marko alikuwa mkubwa na Stefano alikuwa mdogo. Marko alikuwa mtu wa kubishana sana na mara kwa mara hakumtii baba yake. Mzee huyu aliwapenda sana watoto wake, na alimwadhibu ye yote ambaye alikosa kutii.

Marko aliendelea kutotii maagizo ya babake, lakini Stefano alisikitikia sana mateso ambayo ndugu yake alikuwa akipata kwa kutotii kwake. Stefano aliamua kuchukua adhabu ya ndugu yake. Alidhania kwamba hii ingemfanya nduguye kutambua makosa yake, atubu na kuyasikitikia na aanze kutii maagizo ya baba yake.

Stefano alitaka ashinde shida iliyoletwa na ndugu yake nyumbani kwao. Hii ingemwezesha Marko kuishi maisha maaminifu, yenye furaha na amani pale nyumbani.

**Maelezo**

Mungu alipomwumba mwanadamu, alimtembelea na kuzungumza naye katika Bustani ya Edeni. Hatimaye mwanadamu alianza kutomtii Mungu. Dhambi iliingia ulimwenguni kupitia kwa mtu mmoja, nayo dhambi ikaleta mauti. Kila mtu alifikiriwa kuwa mwenye dhambi. Soma Warumi 3:23.

Mungu alimpenda mwanadamu hata ingawa alikuwa mwenye dhambi, Alifanya mpango wa wokovu wa mwanadamu ili arudishe urafiki kati yao, naye mwanadamu angeishi maisha mema na yenye maana mbele za Bwana. Watu walikuwa wakitoa dhabihu ya wanyama kabla ya Yesu kufa msalabani. Lakini Mungu aliahidi kutuma Mwokozi kulipa deni la dhambi za ulimwengu. Yohana Mbatizaji alijua jambo hili na





# YESU ANAANZA HUDUMA YAKE

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza jinsi Yesu alivyoanza huduma yake, na jinsi Yohana Mbatizaji alivyomtayarishia njia.

SOMO KUTOKA: Yohana 1

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 1:19-34

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Nami nimeona, tena nimeshuhudia ya kuwa huyu ni Mwana wa Mungu" (Yohana 1:34).

**KUSOMA SOMO**

**Utangulizi**

Je! unakumbuka jinsi ulivyojisikia siku ya kwanza kwenda shuleni? Pengine unakumbuka ukijivunia sana mavazi rasmi uliyokuwa umevaa. Pengine ulikuwa na viatu vipya vilivyong'aa sana. Pengine unakumbuka ukiwa mrefu au mfupi kuliko watoto wengine darasani mwako.

Sasa unakumbuka siku yako ya kwanza kuingia shule ya sekondari? Pengine baadhi ya fikira zile zilikujia akilini. Wakati huu ulitambua kwamba ulikuwa na wajibu mkubwa sana kwa nafasi yako katika shule ya sekondari. Ungepaswa kusoma kwa bidii ili kufanya vizuri. Wavulana na wasichana wengine pia wangekuwa wanangojea kufanya vyema.

Je! ulifikiria baadhi ya wanafunzi wengine ambao wangekuwa rafiki zako? Je! ulifikiria jinsi utakavyo wapendeza? Je!

ulifikiria jinsi watakavyoanza kwa njia nzuri? Kuanza kwa njia nzuri ni jambo kuu sana katika ujiendelezaji wa kazi ya mtu.

Yesu alikuwa na miaka thelathini alipoanza huduma yake. Ilikuwa muhimu sana kwake kuanza kwa njia nzuri. Mungu alimtuma mtu aitwaye Yohana, ambaye alikwua wa mbari ya Yesu, kutayarisha njia kwa kuja kwake. Soma Luka 1:8-17. Mtu huyu aliitwa Yohana Mbatizaji, kwa sababu aliwabatiza watu wengi kama ishara yao ya kutubu dhambi.

**Maelezo**

Soma Yohana 1:6. Mungu alimtuma mtu aliyeitwa Yohana. Kifungu cha 7 kinatwambia kwamba kazi ya Yohana ilikuwa kuishuhudia ile nuru, na Yesu alikuwa nuru hiyo. Yohana aliwaambia watu kwamba Yesu yuaja.

Siku hizo barabara hazikuwa na lami wala nzuri. Watu walianza kutengeneza njia na kunyoosha mapito yake walipopata ujumbe kwamba mfalme au mtu mashuhuri alikuwa anapanga kuzuru wilaya fulani. Siku hizi wakati afisa mashuhuri anapopanga kuutembelea mji fulani, mtu humtangua na kutayarisha njia yake. Watu huambiwa habari za kuja kwake, nao hujitayarisha kumlaki.

Yohana Mbatizaji alikuwa mtangulizi wa Yesu. (Luka 1:5-25, 56-58)

Alianza huduma yake ng'ambo ya Mto Yordani, na akahubiri juu ya tabia ya dhambi na kuwabatiza watu. Haya ndiyo matayarisho ambayo watu wangefanya kwa ajili ya kuja kwa Masihi.

Soma Yohana 1:19-28. Watu walimwuliza Yohana mara kwa mara kuwa yeye ni nani. Walidhani kwamba pengine yeye ndiye Masihi. Je! Yohana aliwajibuje? Tazama vifungu vya 20-23. Yohana hakudai kuwa kitu cho chote ila sauti ya



2. Yuda, mwanafunzi wa Yesu alimsaliti. Je! ni nini kilichomfanya kutenda hivyo?

3. Petro alikuwa amempenda Yesu sana. Je! ni kwa nini alimkana?

4. Jifikirie wewe mwenyewe. Je! wakati mwingine huwa unamkana Yesu? Je! unafikiri unapaswa kufanya nini?

5. Omba kwamba utamfuata Yesu bila kujali mateso yako ya ulimwengu huu.

6. Omba kwamba Mungu atakupa nguvu za kusimama imara katika yeye na kwamba mapenzi yake yatafanyika maishani mwako.

SOMO LA KUMI NA MBILI

# YESU ANASULIBIWA

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba Yesu alikufa msalabani kwa sababu ya dhambi zangu.

SOMO KUTOKA: Yohana 19:28-42

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 19:28-42

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Basi Yesu alipokwisha kuipokea ile siki, alisema, Imekwisha. Akainama kichwa, akaisalimu roho yake" (Yohana 19:30).

kumpenda kila mtu tunayekutana naye na tushiriki masikitiko na wale wenye shida.

Wakati mwingine watu wa ulimwengu hugeuka na kuwa adui zetu badala ya kuwa rafiki. Wakristo wafanyapo yale ambayo watu wa ulimwengu hawataki, huwa wanawaacha. Huwa wanatukana lakini sisi kama Yesu, tunapaswa kuwa waaminifu katika kazi ya Bwana. Mara kwa mara huwa si rahisi kufanya mapenzi ya Mungu, lakini tunapaswa kujitoa kwa mapenzi yake.

Yesu anajua shida ambazo Wakristo wanapata hapa duniani. Hata hivyo, alituwekea mfano wa kufuata. Aliushinda ulimwengu, "Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo, mimi nimeushinda ulimwengu" (Yohana 16:33).

Katika Yohana 17:14-15, twaona kwamba sisi si watu wa ulimwengu huu. Sisi ni kama waamini katika Yesu. Tunashiriki pamoja naye katika chuki ya ulimwengu. Lakini Yesu alidhihirisha hali na kazi yake ya maisha ndani yetu. Tunapokutana na majaribu au hata mateso, tunapaswa kuvumilia bila kudhoofika kwa imani yetu.

Petro alimkana Bwana na akasikitika na kuona hatia yake baadaye. Alimwomba Mungu naye akasamehewa. Wakati mwingine huwa tunamkana Mungu kwa mambo mengi. Hata huwa tunaona haya kuitwa Wakristo, lakini tunapokiri na kutubu kwa Bwana atat urudisha tena katika jamaa yake. Tunapaswa kufanya yale anayotuamuru tufanye.

**Kazi ya Kufanya**

1. Yesu alikuwa amefanya mambo mengi mema, lakini Wayahudi walitaka kumshika. Je! unafikiri ni nini kilichowafanya watake kutenda hivyo?



kuwaelekeza watu kwa Masihi. Alitaka wajue kwamba Mwokozi wao amekuja, na alitaka wajitayarishe kumlaki. Yohana hakujitakia heshima kutoka kwa watu. Alitaka kuwaongoza kwa Yesu.

Lakini kulikuwepo na swali kubwa ambalo liliwatatanisha watu wengi. Kwa nini Yohana alikuwa akibatiza? Walimngojea Masihi kuwabatiza watu. Walimngojea Eliya kuja kutayarisha njia, na iwapo Yohana alikuwa Eliya, basi angebatiza. Lakini Yohana alisema kwamba hakuwa Eliya, wala hakuwa Masihi.

Zaidi ya hayo, Wayahudi waliona kwamba hawahitaji ubatizo. Hilo lilikuwa hitaji la Watu wa Mataifa. Wayahudi walikuwa watu wa Mungu, na hawakuhitaji utakaso, ambao walidhania ndilo kusudi la ubatizo. Yohana alikuwa akiwaambia Waisraeli wafanye kile ambacho Watu wa Mataifa walihitaji kufanya.

Yohana aliwaambia watu hao kwamba ni lazima watubu dhambi zao na wabatizwe. Hakumwachilia huru mtu ye yote. Alihubiri kwamba kila mtu anapaswa kutubu dhambi zake.

Yohana hakuwaruhusu watu waamini kwamba yeye ndiye Masihi.

Soma Yohana 1:29-34. Yohana alisema kwamba anabatiza kwa maji, lakini yule ajaye ambaye watu hawajamtambua, atabatiza kwa Roho Mtakatifu. Yohana alisema kwamba yule ajaye ni mkuu kuliko yeye.

Alikubali kwamba hata hakustahili kulegeza kamba za viatu vyake yule ajaye. Yohana hangeweza kupata kazi ya chini sana kuweza kuelezea alichomaanisha. Ilikuwa kazi ya watumwa kufanya yaliyo na uchafu kama kuvua viatu kutoka miguuni mwa mabwana zao. Lakini Yohana alisema wazi kwamba hakustahili kumfanyia Yesu kazi hiyo.

**Mafunzo ya Sura Hii Kwangu**

Yohana alijua Yesu ni nani, na aliwataka watu wengine wamfahamu. Hatuwezi kumwelekeza mtu mwengine kwa Yesu iwapo sisi wenyewe hatumjui. Je! unajua Yesu ni nani? Je! unamjua kama Bwana na Mwokozi wako?

Je! unaelewa kwa nini Yesu alikuja duniani na kuishi kama mwanadamu? Alikuja kufia dhambi zako. Alikuja kukupatia wokovu. Ni lazima upokee tu wokovu huo kama karama yake kwako.

Yohana alifanya yale ambayo kila mwamini aliyezaliwa mara ya pili anapaswa kufanya kila siku. Alijaribu kuwasaidia watu wengine kujua Yesu yu nani na kwa nini alikuja duniani. Alimtaka kila mtu kujua kwamba ni lazima watubu dhambi zao na wakubali msamaha wa Yesu. Baada ya kutubu na kusamehewa, mwamini mpya anapaswa kubatizwa kama ishara ya maisha mapya aliyoanza. Ubatizo hautamwokoa mtu lakini utauonyesha ulimwengu kwamba mtu huyo ameokoka.

Je! utamwamini Yesu leo kama Bwana na Mwokozi wa maisha yako? Je! utakuwa mwaminifu kuwatayarisha watu wengine njia kupata kumjua pia?

**Kazi ya Kufanya**

1. Je! ni baadhi ya njia zipi ambazo Yohana Mbatizaji alimwelezea Yesu kwa watu ambao hawakuwa wakimjua?

2. Je! Yohana aliwataka watu wafanye nini kabla ya kuwabatiza?

3. Jifunze Kifungu cha Kukumbuka na ukikariri kila asubuhi kabla ya kutoka kitandani.

4. Mwombe Mungu akuonyeshe jinsi uwezavyo kutayarisha njia kwa ajili ya kuja kwake moyoni na maishani mwa mtu



majaribu ulipofika. Wanafunzi wake wote walimwacha Yesu afe peke yake.

Yesu alijua kwamba alikuwa akienda kumfia mwanadamu, alipaswa anywee kikombe ambacho Mungu alikuwa amempa. Kwa hivyo, alijiruhusu kushikwa. Alikuwa na uwezo wa kuzuia kushikwa huku, lakini alitaka kutimizwa kwa mapenzi ya Mungu. Twaona katika Isaya 53:4-5 kwamba yalikuwa mapenzi ya Mungu kwa Yesu kufa ili kulipa deni la dhambi zetu. Mwili wa Kristo ulipaswa uwe dhabihu. Wayahudi walitoa dhabihu ya wanyama ambayo haikutosha kamwe kutakasa na kusafisha dhambi. Hata twaona katika Yohana 18:4-5 kwamba Yesu alijitoa mwenyewe kwa askari wa Kirumi. Askari hawakuamini kwamba angejitoa hivyo kwao. Yesu alijua kwamba wanafunzi wake watatawanyika na kumwacha peke yake saa ya mwisho itakapowadia. Soma Yohana 16:32. Lakini katika haya yote Yesu alikuwa tu mwaminifu kwa kukamilisha kazi yake.

Baada ya kifo cha Yesu na kufufuka kwake, aliwatokea wanafunzi wake mara nyingi. Alitaka ahakikishe kwamba neno la Mungu litaendelea kuenea ulimwenguni kwote alipojua kwamba atapaa na kwenda mbinguni. Twaweza kuona vizuri katika Yohana 21:15-17 kwamba Yesu alitaka kurudisha hali ya Petro ya kuwa mwanafunzi. Alihitaji toba ya upendo ya aina tatu. Kila kukiri kwa Petro kulifuatia na agizo la Kristo kwamba, "Lisha wana-kondoo wangu." Yesu alimtaka Petro atimize agizo lake bila kuruhusu kitu kingine cho chote kukatiza jukumu lake. Baadaye Petro alikuwa mmoja wapo wa viongozi wakuu wenye ujasiri wa kanisa la kwanza.

**Mafunzo ya Sura Hii Kwangu**

Watu wote ni wageni hapa ulimwenguni. Sisi huwa na marafiki wengi wema. Nasi kama Wakristo tunapaswa

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

Je! umewahi kuona vibaya baada ya kuwa na rafiki ambaye mwishowe alikugeuka na kukudanganya? Hili ni jambo la kusikitisha sana. Huwa tunaacha kumwamini mtu huyo. Yesu alijua sikitiko la mtu mmoja anayemsaliti kwa maadui zake na rafiki yake mwengine ambaye alikana kwamba hamjui kamwe. Tendo la msalaba lilikuwa jambo ambalo lilileta uchungu mwingi, naye Yesu hakutaka kuteseka hivyo. Lakini kusalitiwa na kukataliwa na rafiki zake kulikuwa mzigo mkubwa zaidi kwake. Hebu jaribu kufikiria jinsi ungesikia ikiwa rafiki zako wangekufanyia jinsi Yuda na Petro walivyofanya.

**Maelezo**

Watu wengi walianza kumfuata Yesu alipofanya miujiza mingi alipoishi hapa duniani. Wayahudi waliogopa kwamba Yesu angechukua vyeo vyao. Hata walitaka kumwua mbali na kufanya mambo mema hapa duniani. Katika Yohana 10:31-33 walisema kwamba Yesu alijifanya kuwa Mungu kwa hivyo alipaswa kufa.

Yuda ambaye alikuwa mwanafunzi wa Yesu aligeuka msaliti, alijua Yesu alikuwa nani, lakini Shetani aliingia moyoni mwake. Katika Yohana 18:5, Yuda anaonekana akiwa amesimama pamoja na askari wa Kirumi walipofika kumshika Yesu.

Wanafunzi wengine wa Yesu walimpenda sana. Walijua alitoka kwa Mungu naye ni Mungu. Petro akiwa kama mfano, aliahidi kutomwacha Bwana hata ikiwa itambidi kufa pamoja naye. Soma Mathayo 26:35. Wakati wa shida ulipofika, Petro alimkana Yesu. Soma Yohana 18:17, 25 na 27. Petro alitaka kwa uaminifu kutetea Yesu, lakini alimkana wakati wa



unayemfahamu. Mwambie kwamba unataka kuwa shahidi mwaminifu kwake.

SOMO LA TATU

# YESU ANATHIBITISHA UWEZO WAKE

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba Yesu alitumia uwezo wake kwa makusudi maalum.

SOMO KUTOKA: Yohana 2:1-25; Mathayo 4:1-7

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 2:1-25

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Yesu akajibu, akawaambia, Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha" (Yohana 2:19).

## KUSOMA SOMO

**Utangulizi**

Ilikuwa saa tano ya usiku, nao wageni walikaribia kumaliza sherehe ya karamu ya kuzaliwa na kwenda zao. Mgeni mheshimiwa alikuwa akisema maneno ya hotuba yake ya mwisho waliposikia hatua za mtu atembeaye akikaribia chumba hicho. Watu fulani waliingia ndani wakiwa wamefunika nyuso zao na kuacha sehemu ndogo ya kuonea. Mmoja wao akasema kwa sauti, "Kila mtu ainue mikono juu!"

Mmoja wa wezi wale aliikaribia meza na kuchukua zawadi na pesa zilizotolewa. Palikuwepo na polisi kati ya wageni walioalikwa. Alikuwa amewaleta baadhi ya rafiki zake katika karamu hiyo. Waliweza kwa haraka kuwazunguka wezi wale

na kuwaamuru kujisalimisha. Chumba hicho kilikuwa tena kitulivu, na watu wakajisikia huru kuweza kupumua.

Yesu alitumia pia uwezo wake kuwasaidia watu. Huwapa furaha wote wanaompokea. Hebu tuufikirie uwezo wa Yesu siku hizi.

**Maelezo**

Katika Yohana 2:1-11 tunaona mfano wa uwezo ambao Yesu alithibitisha alipohudhuria arusi huko Kana. Mariamu, mamake Yesu, alikuwa ametoka Nazareti kuhudhuria arusi hiyo, lakini palitokea shida. Divai ilikuwa imekwisha. Hii ingekuwa chukizo kubwa kwa bwana na bibi arusi.

Tazama kifungu cha 4 kuona sehemu ya Mariamu katika lile ambalo lingetokea. Alimwendea Yesu kumwomba msaada kwa sababu alijua kwamba alikuwa na uwezo maalum ambao ungesuluhisha tatizo hilo.

Yesu aliwaambia watumishi kujaza maji mitungi hiyo sita. Walipotii na kujaza, aliwaambia sasa wachote kutoka kwa mitungi hiyo na wampelekee msimamizi wa karamu. Mtu huyu hakuwa akifahamu kwamba palikuwepo na tatizo. Wakati msimamizi alipoionja divai, alisema kwamba ilikuwa bora zaidi kuliko ile aliyokunywa mbeleni.

Huu ndio mwujiza wa kwanza ambao Yesu alifanya wakati alipoishi duniani.

Baadaye Yesu alikwenda hekaluni huko Yerusalemu. Alichukizwa sana alipowaona wafanya biashara na wavunjaji pesa wakiuza hekaluni. Walikuwa wakiwavunjia fedha watu waliotoka mbali na kuuza ng'ombe, kondoo na njiwa kwa ajili ya dhabihu ambayo wangetoa. Yesu alikasirika sana. Aliwatoa wote katika hekalu akisema, "...Yaondoeni haya; msiifanye



2. Wafikirie washiriki wa kanisa lako. Je! kunao wale ambao wana mzigo wa hofu na mashaka? Je! ni kwa nini wana mashaka haya? Je! unaweza kuwaambia nini?

3. Omba kwamba Mungu ataondoa hofu na mashaka maishani mwako na atakuhakikishia amefanya kila jambo kukutayarishia njia.

4. Omba kwamba Mungu atakufanya uelewe hasa kwamba alimtoa Roho Mtakatifu kabla ya kuondoka. Omba kwamba atakupa nafasi na hekima ya kushiriki na wengine yale aliyotoa ili waweze kumwamini na kumtegemea Bwana kwa kila jambo.

SURA YA KUMI NA MOJA

# YESU ANASALITIWA NA KUKANWA

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba kila mmoja alimwacha Yesu afe peke yake, lakini alikuwa mwaminifu kukamilisha kazi aliyokuja kufanya.

SOMO KUTOKA: Yohana 18:1-2,17,25-27; 21:15-17; Mathayo 26:75; 27:3-5

VIFUNGU VYA LEO: Vyote Hapo Juu

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Basi Yesu akamwambia Petro, Rudisha upanga alani mwake; je! kikombe alichonipa Baba, mimi nisikinywee?" (Yohana 18:11).

tumwamini Yesu Kristo kupitia kwa Roho Mtakatifu kwa kupata suluhisho. Yesu aliposema, "Msaidizi mwingine" alimaanisha kwamba Roho Mtakatifu angefanya jinsi yeye mwenyewe alivyofanya alipokuwepo kimwili hapa duniani.

Yesu hataki tuwe na hofu wakati tuwapo na shida. Anataka tumwamini. Ni lazima tumwamini. Mungu ni mwaminifu, nasi huonyesha uaminifu na utiifu wetu kwake tufanyapo mapenzi yake. Ni lazima tumtukuze Mungu kupitia kwa Roho wa Mungu.

Roho Mtakatifu yuko ndani yetu milele. Yeye ni roho wa kweli wa Bwana ambaye Yesu aliahidi. Anauwezo wa kutufanya tushinde dhambi na majaribu. Katika 2 Wathesalonike 2:7 maneno haya, "...lakini yuko azuiaye sasa,..." yanamaanisha Roho Mtakatifu ndiye ambaye anaendelea kutupa uwezo. Yeye hufanya pia mambo mengine mengi maishani mwetu, "Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia" (Yohana 14:26). Ni lazima tumtegemee Roho Mtakatifu aliye maishani mwetu jinsi atakavyotuongoza, na kutufariji, na kutufundisha na pia kutusaidia. Atatukumbusha yale yote ambayo Yesu alisema. Tutagundua kwamba Yesu hakutuacha peke yetu. Alituachia Roho Mtakatifu kabla ya kurudi tena mbinguni.

**Kazi ya Kufanya**

1. Mfikirie mshirika wa kanisa ambaye amepata shida maishani. Amekata tamaa na sasa ametegemea mambo ya dunia kwa kusuluhisha shida zake badala ya kumtegemea Mungu. Je! unafikiri ni kwa nini amefanya hivyo.



nyumba ya Baba yangu kuwa nyumba ya biashara" (Yohana 2:16).

Kule jangwani tulimwona Yesu akiwa mwenye njaa, lakini hakutumia uwezo wake kuyafanya mawe kuwa mkate. Soma Mathayo 4:1-7. Shetani alijaribu tena kumshawishi kufanya jambo lisilo la kawaida la kuruka kutoka juu sana. Kisha akamwambia kwamba Mungu atawatuma malaika kumlinda Yesu asije akaumia. Lakini Yesu hakufanya hivyo. Hakutumia uwezo wake kwa faida yake mwenyewe, lakini hakuacha kuitumia kuwasaidia wengine wenye mahitaji. Yesu anauwezo wote, lakini hakuutumia kamwe vibaya.

**Mafunzo ya Sura Hii Kwangu**

Je! una uwezo wo wote? Kwa kweli huna uwezo jinsi Yesu alivyokuwa nao. Hakuna aliye na uwezo huo. Lakini Mungu anampa kila mtu uwezo wa kufanya kazi ambayo anamtaka afanye. Je! utafanya nini na uwezo wako?

Tunapaswa kujifunza kutoka kwa mfano wa Yesu kwamba uwezo wo wote tunaopewa hatupaswi kuutumia kwa faida yetu wenyewe. Hutupa kile tunachohitaji kufanyia kazi fulani. Ni lazima tuutumie vizuri uwezo huo.

Huwapa baadhi ya watu uwezo wa kufundisha wengine. Wengine wanaweza kutibu ugonjwa, hali wengine wanaweza kujenga barabara au nyumba. Ni lazima kazi ambayo Mungu anaiweka mikononi mwako uifanye vizuri uwezavyo, hata kama ni nini. Hupaswi kuwa na wazo la faida ya kibinafsi zaidi ya malipo maayokubaliana.

Unawezaje kuwa na uhakika kwamba utatumia uwezo wako kwa njia inayofaa? Ni lazima uwe na ushirika mwema na Mungu, Baba yako wa mbinguni. Ni lazima utambue kwamba yeye ni Mungu, na ni lazima umwabudu kila wakati.

Kumbuka kwamba ni Mungu ambaye amekupatia vyote ulivyo navyo. Alikupa uwezo wote ulionao. Alikupa nafasi yo yote ya kumhudumia. Ni lazima uwe tayari kumpa maisha yako kwa kumhudumia na kwa upendo.

Jua kwamba huna uwezo wewe mwenyewe. Uwezo wote hutoka kwa Mungu. Unaweza kufanya mambo yote anayokutaka ufanye, lakini kazi yake inamtengemea yeye. Bila yeye huwezi ukafanya cho chote. Soma Yohana 15:5.

Je! umewahi kuona tracta ikilima shamba? Ni lazima iwe na nguvu. Huwa inapataje nguvu za kufanya kazi? Ni lazima kuwekwe mafuta na petroli.

Nawe pia unapaswa kupata nguvu zako kutoka chanzo kimoja. Yesu ndiye chanzo hicho. Atakupa nguvu iwapo utakaa ndani yake. Soma Yohana 15:7.

Je! utampokea Yesu leo kama Bwana na Mwokozi wa maisha yako? Je! utamwomba akupe nguvu na uwezo kuishi maisha anayotaka uishi?

**Kazi ya Kufanya**

1. Anza kila siku kwa kukariri Kifungu cha Kukumbuka, Yohana 2:19. Je! Yesu alimaanisha nini aliposema kwamba "...livunje hekalu..."?

2. Fanya orodha ya wakati ambapo Yesu alitumia uwezo wake maalum kuwasaidia watu wengine.

3. Hebu yafikirie maisha yako. Utatumiaje uwezo na nguvu zako kuwasaidia watu wengine? Andika njia hizo.

4. Fikiria chanzo cha nguvu na uwezo wako. Je! huwa na wakati na Yesu kila siku kumruhusu akupe nguvu kwa kile anachokutaka ufanye siku hiyo? Panga muda kila siku ambao utazungumzana na Yesu. Tumia wakati huo kusoma Neno



ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6).

Yesu alitoa wokovu, tumaini la uzima wa milele na Roho Mtakatifu kabla ya kuondoka. Damu yake ilitoa wokovu kwa watu wote aliposulibiwa msalabani. "Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu" (Yohana 12:32). Kifo na kufufuka kwake vilitoa tumaini la uzima wa milele. Alifanyika njia ya kumwendea Baba kwa wote ambao wangempokea. Aliwapa Roho Mtakatifu. Katika Yohana 20:22, aliwavuvia pumzi na kuwaambia, "...Pokeeni Roho Mtakatifu" hapo alidhihirisha kwamba pumzi na uwezo wa Roho Mtakatifu hutoka kwake. Baada ya kupokea Roho Mtakatifu aliwaagiza kwenda na kungojea kujazwa a uwezo wa Roho Mtakatifu. Soma Luka 24:49. Kuanzia hapo, wangekuwa sasa mashahidi wa Yesu Kristo. Roho Mtakatifu, angewaongoza, na kuwapa furaha, na kuwafariji na kuwasaidia kufanya mapenzi ya Mungu.

**Mafunzo ya Sura Hii Kwangu**

Yesu Kristo alikaa na wanafunzi wake kwa muda wa miaka mitatu. Wakati ulikuwa umefika wa kuwaacha na kwenda mbinguni. Alipaswa kuwaelezea yote ambayo yangetokea kwake kabla ya kuondoka. Aliwaambia habari za kusulibiwa kwake, kufa, kuzikwa na kufufuka. Alisema kwamba angepaa juu mbinguni na angewaletea mfariji.

Yesu hataki tupate shida kwa sababu ameenda mbinguni. Anatupenda na siku moja atatupeleka nyumbani kwake, mbinguni. Kwa hivyo mfariji, Roho Mtakatifu ambaye alimtuma, atatusaidia hapa duniani. Kuwa na Roho Mtakatifu ndani yetu ni sawa na kuwa na uwepo wa Yesu Kristo. Yesu alisema kwamba, "Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele" (Yohana 14:16). Wakati tunapopatwa na shida na matatizo, ni lazima

mtu wa kufanya kazi hiyo yake wakati atakapoondoka. Stefano angewatunza na kuwaongoza jamaa yake yote.

Kabla ya Andrea kuondoka aliwapa maagizo jamaa yake. Aliwaambia kwamba wanapaswa kumtii na kumwamini Stefano, na wanapaswa kuendelea na upendo walio nao. Wakifanya hivyo, wataishi kwa furaha hadi arudipo tena na kushiriki nao kwa furaha kuu.

Hatimaye Andrea aliondoka na kwenda nchi nyingine. Stefano alifika na kuchukua wajibu wa kuiongoza jamaa hiyo, na hakukuwa na matatizo ambayo hangeweza kusuluhisha. Andrea aliporudi alipata kwamba jamaa na nyumba yake ilikuwa imetunzwa vyema jinsi alivyoiacha.

**Maelezo**

Yesu Kristo aliwatimizia wafuasi wake kabla ya kuondoka duniani na kurudi katika kiti cha enzi cha Baba yake kule mbinguni. Kabla ya kuondoka aliwaambia wanafunzi wake kwamba baada ya siku chache kupita hatakuwa tena pamoja nao. Hawangeenda kule anakoenda wakati huo, lakini wangeenda baadaye. Soma Yohana 13:31-35.

Jambo hili liliwaletea mashaka wanafunzi wake. Twaona katika Yohana 14:1-2 kwamba wanafunzi wa Yesu walikuwa na mashaka na hofu kuhusu kusalitiwa kwa Yesu Kristo na kubashiri kwake juu ya kifo chake. Yesu aliwaambia kwamba hawapaswi kuwa na hofu kwa kuwa alikuwa akienda kuwatayarishia makao. Makao haya, mbinguni, yana vyumba vingi na hutoa nafasi kubwa ya matendo ya furaha kati ya Wakristo waaminifu. Katika kifungu cha 4, ilikuwa muhimu sana kwa wanafunzi wa Yesu kujua njia ya kumfuata kuliko kujua habari za makao. Walipaswa kuamini, kutii na kumwamini kama njia ya pekee ya kwenda mbinguni. "...Mimi



lake na kuzungumzana naye. Hakikisha kwamba unasikiliza anaposema nawe.

5. Omba kwamba Mungu atakupa nguvu za kushinda majaribu ya Shetani kila siku.

SOMO LA NNE

# YESU ANAFUNDISHA KUHUSU KUZALIWA UPYA

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kile Yesu alichofundisha kuhusu kuzaliwa upya.

SOMO KUTOKA: Yohana 3:1-18; 7:50-51; 19:39

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 3:1-18; 7:50-51; 19:39

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "...Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu" (Yohana 3:3).

**KUSOMA SOMO**

**Utangulizi**

Daudi, kijana mwanafunzi alitamani kupata kitu cha kujaza upweke ulioko maishani mwake tangu alipoingia shule ya kulala. Alikuwa amefurahia, Shule ya Jumapili na ibada alipokuwa nyumbani. Rafiki zake wote walikuwa huko, lakini hapa wanafunzi wengi walimchekelea sana yeye na wengine waliookoka.

Yakobo alikuwa Mkristo, kwa hivyo Daudi aliamua kumjaribu, "Yakobo, utapataje mke?" Pengine alifikiri kwamba, akimwonyesha Yakobo kuwa ni mjinga kwa kukubali dini ya mzungu basi wengine watamkubali. Lakini alijua moyoni mwake kwamba hakufikiria sawa.

Alisoma sana Biblia, na akazidi kufanya vizuri darasani. Hata alijaribu kuonyesha kwa vitendo yale aliyosoma. Lakini aliwaza alipolala kitandani mwake usiku, "Nitafanyaje? Je! nina tumaini lo lote? Nataka kufanya mapenzi ya Mungu, lakini sikubaliki katika makundi haya."

Vijana wengi wana shida hii, lakini Yesu anajibu.

**Maelezo**

Habari zilikuwa zimeenea Yerusalemu yote na nchi jirani za mtu kutoka Galilaya, mwana wa seremala, ambaye alikuwa akifanya miujiza na kufundisha mambo ya ajabu. Nikodemo, Mfarisayo, alitaka kukutana na mtu huyu. Nikodemu kama Mfarisayo, alikuwa mfuasi wa dini, aliyeheshimiwa na alielimika sana na maandiko. Alikuwa mmoja kati ya wakuu, kamati ya watu sabini iliyosimamia mambo ya dini na tabia za Waisraeli. Je! ni wakati gani ambapo angewmendea Yesu? Usiku ungefaa kwa sababu hangeonekana na watu. Yeye kama mwalimu alitarajiwa kufahamu mambo yote yanayohusu ufalme wa Mungu, lakini hakuelewa yote.

Katika kifungu cha 2, Nidodemo alisema, "...twajua...." Hakutaka kujitambulisha peke yake kwa Yesu. Lakini hii inaonyesha ukubaliano wake kuwa Yesu ni mwalimu kutoka kwa Mungu. Yesu alifahamu shida ya Nikodemo hata kabla ya kuendelea zaidi. Kuutafuta ufalme wa Mungu inamaanisha kuuingia, kuumiliki na kufurahia amani, furaha na maana ya maisha jinsi Mungu alivyokusudia wakati wa uumbaji. Jibu



4. Omba kwamba Mungu akusaidie uelewe zaidi kuhusu ushindi wake juu ya kifo na mauti.

5. Omba kwamba atakupa nafasi ya kuwasaidia watu wengine na kuwafariji ili wasiogope kifo. Mwombe pia akupe ujasiri na hekima unaposhirikiana nao.

SURA YA KUMI

# YESU ANAMTUMA MFARIJI

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba Yesu aliwatimizia wafuasi wake kabla ya kurudi mbinguni.

SOMO KUTOKA: Yohana 14

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 14:1-4

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi" (Yohana 14:1).

**KUSOMA SOMO**

**Utangulizi**

Andrea alifanya kazi kwa bidii akitimiza wajibu wake kwa jamaa yake. Siku moja alipaswa kusafiri hadi kwa nchi nyingine kutimiza kazi fulani ambayo ilikuwa ya muhimu sana kwa jamaa yake. Alipaswa kuieleza jamaa hiyo mipango yote kwa sababu ilibakia siku kidogo aondoke.

Walisikitika sana na kuingiwa na hofu kwa sababu aliwatunza vizuri sana. Hata hivyo, Andrea aliwaambia kwamba atamleta

hapati faida yo yote akipata mambo yote ya duniani na kuipoteza milele roho yake. Mathayo 6:33 inasema kwamba, "Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa." Mwamini anapofanya hivyo, hupata ushindi juu ya Shetani na dhambi.

Kufufuka kwa Yesu ndio msingi wa maarifa ya Mkristo. Kristo ana uwezo juu ya mauti. Wasiowaamini wanajua kifo ndicho mwisho wa maisha. Hapa ndipo chazo cha huzuni wakati mmoja katika jamaa anapokufa. Hawana tumaini la kuonana naye tena.

Wanafunzi wa Yesu waliona hivyo wakati Yesu alipokufa. Hawakuwa wameelewa kwamba angefufuka tena, na wakahisi uchungu wa kutengana naye.

Mungu alitupangia maisha ya ushindi. Hatupaswi kuwa na woga wa mauti. Alitaka tuwe na maisha ya furaha hapa duniani na hata katika uzima wa milele. Alitayarisha njia ya kufanya jambo hili kupitia kwa Mwanawe, Yesu.

Tumaini hili la uzima wa milele ni la waamini wote, na Mungu anawataka washiriki na ulimwengu wote. Si mapenzi yake kwamba mtu ye yote aangamie bila tumaini la kuishi tena.

**Kazi ya Kufanya**

1. Hebu fikiria msiba wa kifo ambacho kilitokea hivi maajuzi katika sehemu unakoishi. Je! kiliwahusuje watu waishipo hapo? Je! walikuwa na tumaini la kumwona tena mtu huyo?

2. Je! kwa nini watu wanaogopa kifo? Umejifunza nini ambacho kitakusaidia kutoogopa kifo?

3. Je! unafikiri kwamba rafiki zako wanajua ushindi wa Yesu kaburini na maana yake kwao? Zungumza na baadhi ya rafiki zako kuhusu jambo hili.



lake lilimtatanisha sana Nikodemo. Soma jibu lake katika kifungu cha 3.

"Amin, amin" ilimaanisha kwamba hapakuwa na njia nyingine ya kuona ufalme wa Mungu ila kuzaliwa mara ya pili, kuzaliwa upya kwa Mungu. Jibu ni kufanywa upya kwa utu wa ndani wa mtu ambaye anaweza kuwa na ushirika na Mungu. (2 Wakorintho 5:17) Hali ya kale ya dhambi (Warumi 3:23) inapaswa kuondolewa.

Kulizuka swali kutokana na mazungumzo haya. Soma kifungu cha 4. Soma pia jibu la Yesu katika kifungu cha 5.

Baadhi ya watu hutumia andiko hili kukubalisha ubatizo wa watoto. Hii haina ukweli wa kibiblia.

Yesu alikuja kuwaokoa wanadamu wanaokufa kwa kufa msalabani. Alitumia kisa kinachofahamika sana kuelezea hali hii. Yesu atainuliwa jinsi nyoka alivyoinuliwa jangwani. Wale ambao watamwangalia kwa imani wataokoka. Tazama Yohana 3:14.

Kuzaliwa kiroho hakukumshangaza Nikodemo. Alijua kazi ya Roho katika historia ya Waisraeli. Alikuwepo wakati wa uumbaji (Mwanzo 1:2), alikuwa ametoa unenaji wa unabii (Hesabu 24:22) na aliwajaza nguvu watu wa Mungu (Kutoka 31:1-2).

Nikodemo alizaliwa upya na akabadilishwa. Siku moja baadaye aliwapinga Wakuu wa dini wakati wa hukumu ya Yesu. Alihatarisha maisha na cheo chake. Soma Yohana 7:50-51.

Baada ya kusulibiwa kwa Yesu, Nikodemo alishirikiana na Yusufu kuuzika mwili wa Yesu. Jambo ambalo halikufanywa na wanafunzi wengine. Alitumia mavazi ya thamani sana kwa

Yesu ambayo yalitumiwa na wafalme. Nikodemo alikuwa tayari kutoa maisha na mali yake kwa ajili ya Yesu.

**Mafunzo ya Sura Hii Kwangu**

Vijana wengi siku hizi hushikilia mambo mengi na kujaribu kuthibitisha kwamba wao ni sehemu ya ufalme wa Mungu. Wanataka kufurahia amani, furaha na ushirika na Mungu ambao aliupangia viumbe wake, lakini hawajampokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wao. Je! baadhi ya watu wanafikiria kuwa nini kitakachowapa baraka hizi?

1. Hekima ya maandiko na kuwa wa dini. Jinsi Nikodemo alivyoona kwamba haitoshi tu kuijua Biblia na kujaribu kuifuata.

2. Kufikiriwa na watu kuwa u mtakatifu iwapo ukweli au sivyo. Mtu huyu huwa anawaza mara kwa mara: "Watu wanafikiria mini ni Mkristo. Itakuaje iwapo nitaliambia kanisa kwamba nataka kuokoka?

3. Wajibu na vyeo vya dini. Mtu huyu anaweza kuwa mwalimu wa Shule ya Jumapili, mkuu wa darasa, msimamizi wa michezo au kiongozi. Watu wengi hujifariji na huduma zao.

4. Kukubali kwamba Yesu ni Mwokozi aliyetumwa na Mungu pia kukubali kazi yake. Watu wengi hukubali wanapoulizwa iwapo wao ni Wakristo, lakini hakuna mabadiliko yo yote maishani mwao.

5. Kusikia mwito wa kushughulikia wokovu. Nikodemo hangeokoka kutokana na kazi yake. Alihitaji imani.

Hakuna kati ya mambo hayo ambalo linaweza kumletea mtu uzao mpya. Ni lazima amwamini Yesu. Ni lazima atubu dhambi zake na aokoke kwa kukubali kifo cha Yesu msalabani kwa ajili ya dhambi zake.



Yesu alikuwa akiomba. Shetani hakutaka akamilishe huduma yake msalabani ya kumwokoa mwanadamu. Lakini Yesu hakufanya dhambi ye yote. Alishinda kwa shangwe kuu.

Yesu alisikia uchungu mkuu msalabani, kisha akasema, "Imekwisha." Yesu alikuwa amemaliza kazi ambayo alikuja kufanya. Alimtengenezea mwanadamu njia ya kupata wokovu.

Yesu alikufa msalabani lakini hakubakia mfu. Alitoka kaburini. Hapa ndipo tunapoona ushindi wake. Hatungekuwa na tumaini iwapo angebakia tu mfu. Yesu alikuwa na uwezo wa kutoa maisha yake na kuyatwaa tena jinsi aliyofundisha katika Yohana 10:18. Hakuna aliyeyachukua kutoka kwake. Alimtukuza Baba yake alipotoa maisha yake. Tazama Yohana 12:27-28.

Yesu alitoa maisha yake na akatoka kaburini kama tunda la kwanza la wale walalao. (1 Wakorintho 15:20-23) Hii inamaanisha kwamba watu wote watakufa, lakini Yesu alikuwa wa kwanza kufufuka kutoka kaburini. Hata hivyo, katika ushindi wake, aliahidi kwamba wale wote watakao mwamini watafufuka pia katika maisha mapya. Tutaishi naye milele kwa sababu yeye yu hai.

**Mafunzo ya Sura Hii Kwangu**

Kifo cha Yesu msalabani kilimaanisha ushindi juu ya dhambi na Shetani. Shetani hakutaka atimize huduma yake ya kumwokoa mwanadamu. Lakini wakati Yesu alipokuwa msalabani alisema kwamba "Imekwisha." Alimaanisha kwamba alikuwa amemaliza kazi ya kumwokoa mwanadamu. Uzima huwajia wale wanaomtafuta na wako tayari kufia maisha yao ya dhambi kupitia kwa kifo, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu.

Hii ni muhimu sana kuliko malengo mengine ya duniani. Inapaswa kuwa ya kwanza juu ya mambo mengine yote. Mtu

Yohana, mwana wa kwanza wa mzee mmoja katika kijiji hicho alikuwa amekufa. Kijana huyu alikuwa mshiriki halisi wa kanisa lao. Alikuwa ameokoka miaka mingi iliyopita na mara kwa mara alizungumzia kuhusu tumaini la wakati ujao. Alikuwa akifanya kazi mjini na kuisaidia jamaa yake.

Kifo kilikuwa na maana tofauti kwa mzee huyu. Hakuwa Mkristo, wala ye yote kati ya jamaa yake waliobakia. Shida yake ilikuwa kwamba hangemwona tena Yohana. Angekosa pia pesa ambazo Yohana aliwatumia nyumbani.

Wakati wa mazishi mzee huyu alimsikia mchungaji akisema kwamba wale waliomwamini Yesu watamwona tena Yohana. Alishangaa maana jambo hili. Mzee huyu alihitaji kujua ushindi wa Kristo.

**Maelezo**

Kifo cha Yesu, kuzikwa na kufufuka vilituonyesha mfano mwema wa maisha ndani yake. Alitumia mfano rahisi kufundisha maana ya jambo hili. Soma Yohana 12:23-28.

Chembe ya ngano inapandwa katika arthi. Kisha inaanza kubadilika, huanza kuota na mmea mpya hutokezea. Mmea huu mpya huzaa ngano zingine wakati wake unapowadia. Lakini kabla ya kufanya hivyo, ngano ya kwanza hupaswa kufa na kutiwa arthini. Hubadilika, wala haiwi tena kama hapo mbeleni.

Vivyo hivyo, Yesu alipaswa kufa ili awalete wengine wengi kwake. Alipaswa kupoteza maisha yake ili mwanadamu apate uzima wa milele. Hakuchagua kuokoa maisha yake mwenyewe. Hakuna mwengine ye yote ambaye angeokoka iwapo angeamua kufanya hivyo.

Kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo kulimaanisha ushindi juu ya dhambi na Shetani. Twaona katika kifungu cha 22 kwamba



Mwanadamu ana uchaguo, kumwamini Yesu na kumwendea kama Mwokozi na kufuata njia zake au kumkana na kuhukumiwa. Je! umegeuka na kumwendea Yesu? Anataka kukuokoa leo.

**Kazi ya Kufanya**

1. Kariri Yohana 3:3.

2. Orodhesha mabadiliko yote ya Nikodemo baada ya kuzaliwa mara ya pili. Orodhesha pia tabia zake kabla ya tendo hili kutokea. Linganisha orodha hizi mbili.

3. Mwambie rafiki jinsi ya kuzaliwa mara ya pili.

SURA YA TANO

# YESU ANASHUHUDIA WENYE DHAMBI

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kuwa shahidi mwema wa Kristo.

SOMO KUTOKA: Yohana 4:3-42

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 4:3-26

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Walakini ye yote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele..." (Yohana 4:14).

**KUSOMA SOMO**

**Utangulizi**

Daudi hakuwa na furaha. Kundi lake la kujifunza Biblia walikuwa wamepanga kwenda gerezani na kuongoza ibada

yao. Wangeimba na kusoma Biblia, na kuomba na kuhubiri. Baadhi yao wangeshuhudia maana ya Kristo maishani mwao. Kiongozi alikuwa amemwambia yeye atoe ushuhuda.

Daudi hakutaka kwenda gerezani. "Watu hao ni wahalifu," akawaza. "Baadhi yao ni wezi, wauaji na wazinzi. Wanaweza wakatudhuru. Hata hivyo, hawastahili kusikia injili. Wala hawastahili kusamehewa."

Daudi alipewa kujifunza yale ambayo Yesu aliwafanyia wenye dhambi. Somo la leo linaonyesha kwamba Yesu aliwashuhudia na akawasaidia kwa njia nyingi. Hata alikuwa ili kuwaokoa wenye dhambi.

**Maelezo**

Ni muhimu kujua msingi wa uhusiano kati ya Wasamaria na Wayahudi iwapo tunataka kuelewa somo hili. Wasamaria walikuwa watu waliokubaliwa kubaki Israeli wakati matajiri na watu mashuhuri waliposhikwa na kupelekwa utumwani, na Ashuru. Soma 2 Wafalme 17:5-6. Waashuru walikuwa wamewaleta kwao mateka wengine. Watu hawa walikuja na sanamu za miungu yao. Hatimaye Wasamaria walianzisha mitindo ya ajabu ya ibada. Walikubali tu vitabu vya sheria, yaani vitabu vya kwanza vitano vya Biblia. Waliabudia tu kwenye hekalu lililokuwa juu ya Mlima Gerizimu.

Wayahudi waliporudi kutoka utumwani, hawakutaka kushirikiana na Wasamaria kwa sababu walikuwa wameoana na watu wa makabila mengine na walifuata na kuabudu miungu ya kigeni. Wayahudi waliomcha Mungu walikataa kabisa kushirikiana na Wasamaria. Hata hawakuweza kupitia katika mji wa Samaria. Wangetembea mwendo mrefu ili kutopitia Samaria.

Lakini Yesu alipitia Samaria. Roho Mtakatifu alikuwa akimwongoza Yesu kwenda mahali ambapo angekutana na



2. Jifunze vizuri Kifungu cha Kukumbuka, na ujue mahali kinapopatikana katika Biblia.

3. Je! unamfahamu mtu ambaye alipata msiba wa kifo hivi majuzi? Shiriki naye baadhi ya vifungu kutoka katika somo hili.

4. Je! kunao watu katika jamaa yako ambao hawamjui Yesu? Waombee na pia ujiombee. Mwombe Mungu akusaidie kuwaonyesha njia ya uzima wa milele.

SOMO LA TISA

# KRISTO MWENYE USHINDI

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza maana ya ushindi wa Kristo juu ya mauti ulivyo kwangu.

SOMO KUTOKA: Yohana 12:1-28

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 12:23-28

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Amin, amin, nawaambia, chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali iyo hiyo peke yake; bali ikifa, hutoa mazao mengi" (Yohana 12:24).

**KUSOMA SOMO**

**Utangulizi**

Jamaa moja ilikuwa na huzuni sana Jumamosi asubuhi. Hawakuwa wakiacha kujiuliza, "Ni kwa nini?" Hata walimlaumu Mungu wakisema kwamba hakuwa kamwe ametenda mema.

nao mwishowe hushindwa. Yesu yungali anataka kuwapa furaha walio na huzuni.

Yesu alishinda mauti na akaondoa uchungu wake. Ye yote asikiaye maneno yake na kumwamini anao uzima wa milele. Hatahukumiwa kamwe. Amekwisha vuka kutoka mautini hadi uzimani. Soma Yohana 5:24.

Unapomwamini Mungu huwa unatambua kwamba hakosi kutimiza ahadi zake kwako. Uwapo na majonzi, yeye atakusaidia kufurahi kwa sababu jina lako limeandikwa mbinguni. Soma Luka 10:20.

Je! umewahi kufiwa na mmoja wa jamaa yenu? Au, umewahi kufiwa na rafiki uliyempenda sana? Huwa na huzuni wakati huo kwa sababu hatapata tena kuwa nawe kama kawaida. Lakini iwapo yeye alikuwa amemwamini Yesu na kumpokea moyoni mwake, basi waweza kuwa na amani na furaha moyoni mwako. Utajua kwamba yeye yuko naye milele.

Unaweza kujua pia kwamba, utakuwa pamoja naye siku moja iwapo wewe pia unaye Yesu moyoni mwako. Kisha utakuja kumwona Yesu na rafiki zako Wakristo. Wewe pamoja na waamini wote mtaishi na Yesu milele. Hakutakuwa tena na huzuni wala utengano.

Hitaji la pekee ni kwamba umpokee Yesu kama Bwana na Mwokozi wako. Je! una uhakika kwamba unayo maisha hayo naye milele.

**Kazi ya Kufanya**

1. Orodhesha vifungu katika Biblia yako ambayo ni vya kufariji wakati wa huzuni na majonzi. Anza na Yohana 11:25; Luka 10:20; Yohana 15:11, Yohana 14:1-4; 1 Wathesalonike 4:13-18.



mwanamke fulani. Ni muhimu kwetu kujifunza kufuata uongozi wa Roho Mtakatifu ili aweze kututumia.

Yesu alipokuwa safarini kwenda Galilaya, alisimama karibu na kisima cha Yakobo pale Samaria mwendo wa saa sita mchana. Alikuwa amechoka sana, na alikaa kwenye mawe ya kisima hicho. Wanafunzi wake walienda mjini kununua chakula.

Mwanamke Msamaria alikuja kisimani kuteka maji. Haukuwa wakati wa kawaida kwa wanawake kwenda kuteka maji. Wengi wao walienda kisimani wakati wa asubuhi au jioni kabisa. Wanawake walifurahia wakati huo ambapo walikutana na rafiki zao walioenda kisimani. Pengine mwanamke huyu alienda tu peke yake kwa sababu alikuwa mwovu. Yesu alimwomba maji ya kunywa.

Mwanamke huyu Msamaria alishangaa sana. Alikuwa ameona Myahudi akiwa Samaria, naye alikuwa akizungumza na Msamaria, hasa mwanamke.

Kisha Yesu alianza kuzungumza na mwanamke huyu habari za maji. Yeye alijua sana habari za maji, lakini alitumia maji haya kwa kuzungumzia habari za mambo ya kiroho.

Soma Yohana 4:3-26. Mwanamke huyu alianza kumwelewa Yesu alipozungumzia kuhusu dhambi zake. Alisadiki na kuamini kwamba Yesu ndiye angeweza kumsamehe dhambi zake. Kisha alienda mbio kijijini kuwaambia rafiki zake kwamba amempata Masihi.

Wao pia walitaka kujifunza, kwa hivyo, Yesu na wanafunzi walikaa katika kijiji hicho kwa muda wa siku mbili na kuwafundisha watu. Watu wengi walimwamini Yesu kwa sababu ya mafundisho hayo.

**Mafunzo ya Sura Hii Kwangu**

Tunapowashuhudia watu siku hizi hatuwezi kujua dhambi ambazo wamefanya. Sisi hatupaswi kujua, lakini Roho Mtakatifu anajua. Yeye atawafunulia dhambia hiyo tunapowashuhudia kwa uaminifu. Jambo la kwanza tunalopaswa kufanya wakati wa kushuhudia ni kumwomba Roho Mtakatifu atuongoze kwa mtu ambaye amemtayarisha kusikia ujumbe wake kwa wakati huo. Kisha tunapaswa kuendelea kumwomba azidi kuzungumzana na moyo wa mtu huyo. Ni yeye tu ambaye anaweza kumthibitishia mtu dhambi zake, na ni yeye tu ambaye anaweza kumwongoza mtu aokolewe.

Utaona katika kifungu cha 20 kwamba mwanamke huyu alijaribu kubishana na Yesu kuhusu mahali panapofaa kuabudia, Yesu alikuwa akizungumzia jambo ambalo lilimpa wasiwasi, kwa hivyo alijaribu kubadilisha mazungumzo yao. Hata aliweza kutumia swali lihusulo dini katika mazungumzo yao.

Lakini Yesu alikataa kubishana naye. Alimwambia kwamba mahali pa kuabudia hapakuwa jambo muhimu. Kilicho muhimu ni roho ambayo mtu anaabudu nayo.

Hata hivyo, katika mafundisho haya, Yesu aliwasaidia watu wote kujua kwamba wanaweza kumwabudu Mungu mahali po pote na wakati wo wote. Tunaweza kumwomba wakati wo wote naye atatusikia. Lakini Yesu alitufundisha kwamba tunapaswa kwenda katika nyumba yake, kanisa, na kaubudu pamoja na watu wake kila mara. Soma Waebrania 10:25.

Ni lazima hata sisi tukatae kubishana na watu wakati tunapowashuhudia. Mabishano yatatufanya tupotezi kusudi letu la kueleza habari za Yesu. Shetani atatufanya tuanze



Wakati Martha aliposikia kwamba rafiki yake, Yesu, alikuwa akija, alienda kumlaki. Alijua upendo mkuu ambao Yesu alikuwa nao kwa ndugu yake, kisha akamwambia, "...Bwana, kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu hangalikufa" (Yohana 11:21). Martha alijua kwamba cho chote ambacho Yesu angemwomba Mungu kingefanyika. Je! hata wewe unaamini hivyo.

"Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi; naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele. Je! unayasadiki hayo?" (vifungu vya 25-26).

Martha aliamini kwamba Yesu alikuwa Kristo, na alijua alikuwa amewarudishia watu wengi uzima na afya nzuri. Hata aliamini katika ufufuo wa "siku ya mwisho." Soma 1 Wathesalonike 4:13-18. Hatimaye Yesu alianza kumfundisha zaidi.

Katika kifungu cha 26 Yesu alizungumzia kuhusu kuishi na kuamini ambayo inamaanisha kwamba mtu anaweza kuwa na utu wa kiroho ambao haufi kamwe. Uzima huu katika Yesu unahitaji imani. Jambo hili lilimfanya Yesu aulize, "Je! unayasadiki hayo?" Ni muhimu kukiri kwa imani na kuamini. Wale wanaomwamini Yesu kama Bwana na Mwokozi wao wataishi naye milele. Soma Yohana 14:2-3.

Itiko la Martha katika kifungu cha 27 linaonyesha ukiri mkuu wa imani, inayomaanisha alielewa kwamba Yesu alikuwa Masihi. Yesu alikuwa tayari kuwarudishia watu waliokuwa na huzuni furaha. Hata nawe waweza kujua furaha atoayo Yesu iwapo utamwamini kama Mwokozi wako.

**Mafunzo ya Sura Hii Kwangu**

Siku hizi watu wengi wanaishi bila tumaini. Wao hujaribu kujitegemea wenyewe kwa kusuluhisha shida zinazowakabili,

Yohana alikumbuka jinsi furaha ya wachezaji ilivyobadilika mara moja na kuwa huzuni. Alikumbuka pia wakati ambapo Yesu alipoibadilisha huzuni na kuwa furaha. Ulikuwa wakati ambapo rafiki yake, Lazaro, alikuwa amekufa. Yesu alimfufua. Kuomboleza kwa dada zake na rafiki zake kulibadilika na kuwa furaha wakati ndugu yao aliporudiwa na uzima.

Hebu tujifunze zaidi leo kuhusu tendo hilo.

**Maelezo**

Je! huwa unafikiria nini wakati mtu asemapo "kifo"? Je! huwa unaifikiria kupotea kwa yule unayempenda? Kifo ni wakati wa majonzi. Twasoma katika Yohana 11:17-27 kuhusu wakati wa huzuni na majonzi katika kijiji kidogo kiitwacho Bethania. Rafiki ya Yesu aliishi huko. Mariamu, Martha na Lazaro walimpenda Yesu, naye aliwapenda na kuwatembelea wakati wo wote alipotaka.

Twaona katika kifungu cha 2 kwamba Mariamu ndiye aliyepaka mafuta miguu ya Yesu na akaifuta kwa nywele zake. Dada hawa walitumana Yesu aje wakati Lazaro alipokuwa mgonjwa. Walijua kwamba Yesu angemponya ndugu yao, kwa sababu alikuwa amewaponya watu wengi.

Lakini wakati huyo Yesu alikuwa Yordani, mahali ambapo Yohana alikuwa amewabatizia watu, katika Yohana 10:40. Palikuwa umbali wa mwendo wa siku mbili kutoka Bethania na Yesu alingojea siku mbili ndipo akaanza safari baada ya kupata ujumbe huo. Wanafunzi walimkumbusha Yesu kwamba watu wanamngojea huko wamwue kwa mawe, lakini Yesu aliendelea na safari yake ya kwenda Bethania. Alipofika aliwakuta watu wakiomboleza kwa sababu Lazaro alikuwa amekwisha kufa. Alikuwa kaburini kwa muda wa siku nne.



kubishana ili atuzie tusishuhudie, lakini ni lazima tumwombe Mungu atusaidie kuepuka jambo hili.

Yesu alianza kwa kuzungumzia habari za kitu ambacho mwanamke huyu alifahamu sana. Kisha aligeuza mazungumzo hayo na kuzungumzia mambo ya kiroho. Alitumia maneno rahisi ambayo mwanamke huyu alielewa kwa haraka. Hakumlaumu kwa ajili ya dhambi zake Hakumwaibisha. Alimwambia wazi kuwa yeye ni nani na kwamba atampa uzima wa milele.

Wakati mwanamke huyu alipoelewa na kuamini kwamba Yesu ndiye Masihi, aliacha mtungi wake wa maji na kurudi mbio kijijini. Aliwaambia rafiki zake habari ya Yesu na akawaleta kwake. Nasi pia tunapaswa kusema kile ambacho Yesu ametufanyia na tuwalete waliopotea kwake.

**Kazi ya Kufanya**

1. Je! kwa nini mwanamke yule Msamaria aliacha mtungi wake aliporudi mbio kijijini kuwaambia rafiki zake kwamba alikuwa amempata Mashihi? Je! unafikiri wangemchelewesha. Je! walikuwa kizuizi kwake kwa wakati huo? Chunguza maisha yake na umwombe Mungu akuonyeshe kile kinachokuzuia kufanya mapenzi yake.

2. Wanafunzi wa Yesu hawakufurahia kupitia Samaria, lakini walipitia huko kwa sababu Yesu alikuwa anaenda huko. Je! unafikiri ni kwa nini hawakutaka kwenda huko? Je! kunaye mtu ambaye hupendi wala kumshuhudia? Kwa nini?

3. Andika orodha ya mambo ambayo unaweza kujifunza kutoka kwa sura hii kuhusu jinsi ya kuwashuhudia wapotevu.

4. Mwombe Mungu akwongoze kwa mtu ambaye amemtayarisha kusikia Neno lake. Mwambie mtu huyo yale ambayo Yesu amekufanyia.

# MAMLAKA YA YESU

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba Yesu ana mamlaka juu ya vitu vyote, hata juu yangu.

SOMO KUTOKA: Yohana 5

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 5:17-29

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Akawajibu, Baba yangu anatenda kazi hata sasa, mimi ninatenda kazi" (Yohana 5:17).

**KUSOMA SOMO**

**Utangulizi**

**Samweli na Paulo walipokuwa wakitembea mjini waliwapata watu watatu wakiwa wamesimama katika kivuli cha jengo moja. Watu hao waliwaamuru walale chini kifudifudi. Wao kwa hofu walifanya jinsi walivyoamriwa na kungojea huku mifuko yao ikipekuliwa.**

Hali hiyo ilibadilika mara moja. Gari lilipinda kona, na wezi hao wakaona kuwa ni la polisi wa kuchunguza eneo hilo. Walianza kukimbia, lakini walishikwa kwa haraka na maafisa wa polisi.

Tangu wakati huo ilikuwa zamu ya wezi hao kuwa kimya, wakisimama, na kukaa, na kutembeatembea jinsi walivyoamriwa na polisi hao. Maafisa hao wa sheria walikuwa na mamlaka ya kuwaambia wale wezi jambo la kufanya.

Yesu alikuwa na mamlaka kutoka kwa Mungu, lakini watu hawakuwa wakitambua mamlaka hayo. Yesu katika sura hii





# YESU, BWANA WA MAUTI

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba Yesu alishinda kifo milele.

SOMO KUTOKA: Yohana 11

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 11:17-27

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi" (Yohana 11:25).

**KUSOMA SOMO**

**Utangulizi**

Kulikuwa na jua kali, na lori ilikuwa imebeba wachezaji wachovu bali wenye furaha sana. Walikuwa wameshinda katika mpira wa miguu, na sasa walizungumzia kuhusu wachezaji waliowafanya washinde. Dreva alishiriki pia katika furaha ya wachezaji, wala hakukumbuka kuna mpinda kwenye barabara hiyo. Lori hiyo iliteleza na kuanguka na kupindukapinduka, mwishowe ilisimama. Ilikuwa imebaki mabati yaliyopondekapondeka.

Kwa ghafla wakati wa furaha uligeuka na kuwa wakati wa maumivu na huzuni. Kila mmoja alianza kulilia msaada na kuwazia hali ya wengine katika gari hilo.

Mtu mmoja aliwaita polisi na gari la wauguzi. Baadhi ya wasafiri wenye magari walisaidia kuwapeleka wachezaji hao hospitalini ambako walitibiwa.

Siku moja watu wote watakufa. Lakini Yesu alisema katika Yohana 11:25-26 kwamba, "...Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi." Wale wanaokufa kimwili huku wanamwamini watakuwa hai kiroho. Hii ndiyo sababu Yohana anaendelea kutwambia kwamba, "Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele..." (Yohana 3:36).

Watu wengi wanafikiri kwamba watu wengine watawapa mambo mema ya maisha jinsi ilivyokuwa na watu wale wanne katika Utangulizi wa somo hili. Lakini ni lazima watu waunganishwe na Yesu kwa imani iwapo watapata uzima wa milele.

**Kazi ya Kufanya**

1. Je! unaelewa nini wakati Yesu aliposema kwamba yeye ni mkate wa uzima?

2. Je! unafikiria ni kwa nini walimkimbia Yesu?

3. Je! kwa nini ilikuwa muhimu kwa Petro na mitume wengine kutoondoka na kumwacha Yesu?

4. Omba kwamba utapata hekima kutoka kwa Mungu na kwamba utawavuta watu wengi kwa Mungu.

5. Omba kwamba wewe na watu unaowaleta kwa Yesu mtajua kwamba Yesu ndiye mpaji pekee wa uzima wa milele.



alijitetea mwenyewe na kuwaambia kwamba yeye na Baba ni mmoja.

**Maelezo**

Ilikuwa siku ya sabato na Yesu alikuwa amemponya tu mtu aliyekuwa kiwete. Mtu huyu alikuwa akingojea karibu na birika la Bethzatha na tumaini la kuponywa. Kuliaminika kwamba maji ya birika hilo yalikuwa na uwezo wa kuponya wakati fulani. Mtu wa kwanza aliyeingia majini humu wakati huo aliponywa. Lakini mtu huyu alikuwa peke yake. Hapakuwa na mtu ambaye angeweza kumsaidia kuyaingia maji wakati huo, wala hangeweza kujiingiza yeye mwenyewe. Yesu alipomwona alijua kwamba alikuwa amengojea kwa muda mrefu bila kuponywa. Yesu akamwambia mtu huyo asimame, ajitwike godoro lake na aende. Soma Yohana 5:1-9.

Twajifunza kuhusu maswali ambayo Wayahudi walimwuliza mtu huyo aliyeponywa katika vifungu vinavyofuatwa. "Je! kwa nini unabeba godoro lako siku ya sabato? Ni nani aliyekwambia ubebe?" Wayahudi waliamini kwamba kila mtu anapaswa kutii sheria ya Musa. Sheria hiyo ilisema kwamba mtu hapaswi kufanya kazi siku ya sabato, na kubeba godoro ilikuwa kazi.

Shida ilikuwa kwamba hawakuamini kuwa Yesu alikuwa Mungu. Hawakufurahi kwa sababu kiwete yule alikuwa ameponywa. Walianza kumlaumu Yesu kwa kumponya mtu siku ya sabato.

Soma jinsi Yesu alivyowajibu katika kifungu cha 17. Wayahudi wote walijua kwamba Mungu aliuumba ulimwengu na kisha kupumzika siku ya saba. Walijua kwamba Mungu anautegemeza ulimwengu, yaani, anauendeleza. Kwa hivyo wangekubali kwamba Baba anafanya kazi. Kazi ya Mungu haisimami kamwe. Wayahudi hawangemshitaki Mungu, mpaji

wa sheria, ya kuvunja sheria. Lakini wangemshitaki Yesu. Kifungu hiki kinatwonyesha kwamba hakuna tofauti kati ya kazi ya Baba na Yesu. Wao ni mmoja.

Twaona katika kifungu cha 18 kwamba hasira na ghadhabu ya Wayahudi ilizidi wakati Yesu aliposema kwamba Mungu ni Baba yake. Hili lilikuwa dai kwamba Yesu ni sawa na Mungu. Kulingana na fikara za Wayahudi hili lilikuwa kosa kubwa kuliko kutotii sabato. Hasa hili ndilo tatizo lililowafanya Wayahudi kumkasirikia sana Yesu. Yohana aliandika kuhusu miaka hii baada ya Yesu kufa msalabani. Kwa hivyo aliweza kueleza kwa nini na sababu iliyowafanya Wayahudi kuwa na chuki kama hii.

Katika Yohana 5:19-29, Yesu anaeleza uhusiano wake na Baba. Ilitoa uthibitisho zaidi wa mamlaka ya Yesu. Yesu alizungumzia juu yake mwenyewe kama Mwana. Hakudai kuwa mkuu kuliko Baba, lakini alidai kuwa sawa naye. Alionyesha kwamba alikuwa mtiifu kwa mapenzi ya Mungu.

Msingi wa uhusiano kati ya Baba na Mwana ni upendo. Soma Yohana 3:16 kuelewa upendo wa Mungu kwa ulimwengu. Mungu anampenda pia Mwana. "Kazi kubwa zaidi kuliko hizo" ambazo angeonyesha ingekuwa miujiza mingine na hata kufufuka kwa Yesu. Ishara hizi zote na miujiza vilifanywa ili watu waweze kuona uwezo wa Mungu na wamwamini Yesu.

Kifungu cha 21 ni unabii wa watu ambao Yesu angewafufua. Yesu ni mpaji wa uzima, sio tu kwa wale aliowafufua katika wafu, bali kwa kila mtu anayemwamini.

Mwana amepewa kazi ya kuhukumu ulimwengu. Tazama kifungu cha 22. Amekuwa hakimu kwa kuja kwake, mrekebishaji ulimwengu. Watu huhukumiwa naye. Hii inamaanisha kwamba hatutahukumiwa milele tuutafutapo msamaha wa wokovu wake. (Yohana 3:18)



ambaye ni mpaji wa uzima wa milele. Maneno ambayo Petro alisema yadhihirisha imani na ufahamu wake.

Baadaye Yesu alisema kwamba yeye ndiye uzima, "...Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6). Yesu ndiye mpaji pekee wa uzima kwa watu wote.

**Mafunzo ya Sura Hii Kwangu**

Yesu alipokuwa Kapernaumu, alijaribu kuwaonyesha kwamba alikuwa mkate wa uzima. Watu wote wanaompokea kama Mwana wa Mungu na Mwokozi wa ulimwengu watapata uzima wa milele. Wakristo wanaposhiriki katika kula mkate na kunywa divai, hufanya hivyo kama ukumbusho wa kufa na kufufuka kwa Yesu. Kwa kufanya hivyo huwa wanaonyesha kwamba damu na mwili wa Yesu hutoa uzima. Katika Yohana 6:35-40, Yesu anajidhihirisha kuwa mpaji wa uzima wa kiroho. Wakristo wamwendeapo Yesu na kumwamini, hutimiza njaa ya kiroho na kiu ya Mungu ambavyo ni hitaji kuu la utu wa binadamu. Baadhi ya watu huenda kanisani kwa sababu ya hitaji la vifaa na mali na kufikiria kwamba watapata kutoka kwa washiriki, mchungaji au mmisheni. Watu kama hawa wanalinganishwa na wale waliomfuata Yesu kwa sababu ya mkate waliokula wakati Yesu alipowalisha watu elfu tano. Biblia inatwambia katika Mathayo 6:33 kwamba tuutafute ufalme wa mbinguni na hayo mengine tutaongezewa.

Maneno ya Yesu Kristo yanapaswa kutimiza mahitaji yetu. Ni maneno yanayotuletea uzima wa milele. Twaona katika Yohana 6:67-69 kwamba Petro alitosheka na mkate wa uzima. Twaona katika Yohana 6:53-54 kwamba watu hawana uzima wa kiroho, ndani yao, wasipoula mwili wa Yesu na kunywa damu yake.

**Maelezo**

Yesu alikuwa amewalisha watu elfu tano, na wengi walimfuata alipovuka ng'ambo ya ziwa la Tiberia. Moyo wake ulijaa huruma, na akaanza kuwafundisha. Alijua kwamba wengi walimfuata kwa sababu ya mkate waliokula na miujiza aliyofanya.

Yesu alianza kuwaambia kwamba yeye ni mkate wa uzima uliotoka mbinguni, na wote watakaokula mkate huo wataishi milele. Twaona katika Yohana 6:60, 66 kwamba watu wengi waliosikia fundisho lake waliona kuwa gumu na wakaondoka bila kumkubali kuwa ni Masihi.

Hata hivyo, huu ndio uliokuwa mwanzo wa ujumbe wa Kristo katika sinagogi la Kapernaumu kuhusu Mkate wa Uzima. Yesu alitaka kuwafanya watu kusikia njaa ya chakula cha kiroho. Alitaka kuwapa uzima wa milele badala ya chakula kiozacho. Watu waliona vigumu kuelewa katika hali ya kiroho yale aliyosema kuhusu kula mwili wake na kunywa damu yake. Mawazo yao hayangeacha kufikiria chakula cha kimwili jinsi ilivyo katika Kutoka 16:4,15.

Wengi kati ya mitume kumi na wawili waliamini kwamba Yesu tu ndiye angepatiana uzima. Yuda Iskariote tu ndiye hakuamini hivyo. Wanafunzi wa Yesu walikuwa na msingi mzuri wa imani kuliko watu wengine wote, na kwa hivyo walibakia imara kwa hilo. Hii inaweza kuonekana wazi wakati watu wengi walipomwacha Yesu na kumkimbia. Yesu aliwauliza wale kumi na wawili, "...Je! ninyi nanyi mwataka kuondoka?" (Yohana 6:67) Petro alimjibu hivi, "...Bwana! Twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele. Nasi tumesadiki, tena tumejua, ya kuwa wewe ndiwe Mtakatifu wa Mungu" (Yohana 6:68-69). Petro na mitume wengine walijua kwamba hapakuwa na mwengine ye yote



Kwa kuwa Yesu na Baba ni mmoja, huwa tunamheshimu Baba tunapomheshimu Mwana. Kukosa kumheshimu Mwana huleta kutomheshimu Baba. Hii ndiyo iliyokuwa dhambi ya viongozi wa Kiyahudi.

Twaona mamlaka ya Yesu ya kutoa uzima katika kifungu cha 24. Huwapa uzima wa milele wote wanaomwamini yeye na Baba aliyemtuma. Uzima wa milele huanza tunapompokea Kristo na huzidi kuendelea.

"Wafu" waliotajwa katika kifungu cha 25 inamaanisha wale waliowafu katika dhambi, wale waliopotea. Wote wamwaminio Yesu wanao uzima.

Katika vifungu vya 28 na 29, Yesu alitoa unabii kuhusu siku za mwisho ambapo kutakuwa na ufufuo wa wafu. Wale ambao hawajatubu na kumpokea Yesu watahukumiwa. Wale waliompokea wataendelea kuishi katika uzima wa milele. Wale "waliotenda mema" haimanishi waliofanya kazi nzuri. Inamaanisha wema wa kuwa na imani.

**Mafunzo ya Sura Hii Kwangu**

Ni lazima tukubali dai la Yesu kwamba yu Mwana wa Mungu, aliye sawa na Baba. Watu hawana tumaini iwapo maneno haya siyo ya kweli.

Baadhi ya watu wanamfikiria Yesu kuwa tu mtu mwema au mwalimu mkuu, lakini wanakataa kumkubali kama Mwana wa Mungu. Hali hii haiwezekani. Yesu hangeweza kudai kuwa mtu ambaye hakuwa.

Tunawezaje kumruhusu Yesu kutumia vilivyo mamlaka aliyonayo maishani mwetu kila siku? Ametupa nafasi ya kuchagua yule wa kutumikia katika upendo wake kwetu. Hatatulazimisha tumruhusu aongoze yale tufanyayo kila siku, kule twendako, na yale tusemayo. Anamamlaka, lakini

anatutaka tumkaribishe maishani mwetu. Ni lazima tumwombe awe Bwana wa maisha yetu.

Tuwapo Wakristo ni lazima tumwombe kila asubuhi na tumwambie tunamtaka atuongoze mchana kutwa. Ni lazima tumwulize atwonyeshe mahali pa kwenda, jambo la kufanya na maneno ya kusema. Atatupa nafasi ya kufanya mambo aliyotuwekea siku hiyo.

Je! ni nani anayetawala maisha yako? Je! unaongoza siku zako au unatambua mamlaka ya Yesu maishani mwako?

**Kazi ya Kufanya**

1. Chunguza ratiba ya wakati (muda) wako wa juma lililopita. Je! ni kiasi gani cha muda ambacho ulitumia na Mungu? Je! ulimwomba kila asubuhi kabla ya kuondoka nyumbani? Je! ni kiwango kipi cha muda ambao ulitumia kwa kusoma Neno lake?

2. Chunguza kazi yako ya wakati huo. Je! ni nani aliyeyatawala maisha yako? Je! ulimwomba Mungu aongoze kila kitu ulichofanya na kusema? Je! ulimwomba akuonyeshe sehemu za kwenda na yale ya kufanya kila siku?

3. Hebu fikiria juma lijalo. Je! ni nani ataongoza maisha yako kwa muda wa siku saba zijazo? Je! ungependa kujitoa kwa Yesu sasa hivi kwamba aweze kuongoza yote ufanyayo? Inamisha kichwa chako na umwambie kwamba unataka awe Bwana wa yote ufanyayo na kusema.





# MANENO YA UZIMA WA MILELE

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba Yesu ndiye mpaji pekee wa uzima wa milele.

SOMO KUTOKA: Yohana 6:59-69; Matendo 4:12

VIFUNGU VYA LEO: Yohana 6:59-69; Matendo 4:12

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12).

**KUSOMA SOMO**

**Utangulizi**

Watu wanne walikuwa wameshitakiwa kotini kwa kuvunja sheria za serikali. Katika hukumu yao walipatikana na hatia na walipaswa wafungwe maisha au walipe faini ya pesa nyingi. Watu wengi waliwasikitikia sana lakini hawakuweza kuwasaidia. Mtu mmoja tajiri alikwenda kotini na akawalipia kiasi cha pesa zilizohitajika na wakaachiliwa huru. Watu hawa walifurahi sana kuwa huru. Walimsifu na kumshukuru mtu huyu aliyewafanya huru na kumfikiria kuwa wa pekee ambaye angewasadiia hivyo.

Yesu ni zaidi ya tajiri huyu, ambaye angelipa deni la dhambi. Tuna uzima wa milele tunapomwamini. Tulifanywa huru kutoka kwa utumwa wa dhambi na tuna uzima wa milele.